# Haki Yako

## Kama mwafirika wa unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kijinsia

United Nations
Office of the Victims' Rights Advocate

2023

# Haki Yako

## Kama mwafirika wa unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kijinsia

Una haki ya kutafuta usaidizi na msahada kutoka kwa Umoja wa Mataifa ikiwa wewe ni mwafirika wa unyanyasaji wa kingono au **ukiukiwaji wa kijinsia** unaofanywa na wafanyikazi wowote wa Umoja wa Mataifa au wafanyikazi wanao husika.

Ulipata unyanyasaji wa kijinsia ikiwa ulishiriki tendo la ngono kwa sababu ulitishiwa, au ulilazimishwa kwa nguvu kufanya hivyo, au kukubali kushiriki tendo hili chini ya hali zisizo sawa, kwa mfano kwa sababu hukuweza kuamua kwa uhuru, au ulisikia woga ya matokeo ya kukataa kushiriki kitendo kama hicho. Kufatana na sheria za Umoja wa Mataifa, ulizulumiwa kingono ikiwa ulishiriki, au uliwahi kufanyiwa, tendo la ndoa ukiwa chini ya miaka 18. Wewe pia ni mwafirika wa unyanyasaji kingono ukiwa ulijaribiwa na mojawapo ya mabaya haya.

Umezulumiwa kingono ikiwa ulihaidiwa au ulipewa pesa, chakula au manufaa mengine yoyote, kama vile nyumba au kazi, kwa malipo ya kushiriki tendo la ngono na wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa au wafanyakazi wanao husika.

Ikiwa umepata **ukiukiwaji wa kijinsia au** unyanyasaji kingono, Umoja wa Mataifa utakusaidia kupata huduma ya matibabu na usaidizi mwingine ambao unaweza kuhitaji na uta tamani kupokea. Pia itakusaidia kupata usaidizi wa kisheria, ikiwa utapendezwa kusaiwa hivyo.

**Vitendo vya ukiukiwaji wa kijinsia na** unyanyasaji kingono haviruhusiwe kwa wafanyikazi wote wa Umoja wa Mataifa na wafanyikazi wanao husika. Vitendo kama hivyo havikubaliki, kwa hali yoyote. Umoja wa Mataifa una mwaajibu ya kupeleka malalamiko ya unyanyasaji wa kijinsia kwa uchunguzi halifu. Umoja wa Mataifa utatumia juhudi zake bora ili aliye tenda tendo la kijinsia ku azibiwa vikali kwa makosa yake. Hii inaweza kuhusisha hatua za ndani za kuazibu au ushirikiano na Nchi Wana memba.

Nyaraka hii inaelezea haki zako, na jinsi Umoja wa Mataifa utakavyo kusaidia.

**Kanuni za mwongozo za Umoja wa Mataifa :**

Haki, mahitaji, usalama na utu wako ni vipaumbele.

Una haki ya kutohukumiwa, kulaumiwa au kuwajibika kwa mazara uliyopata kutokana na unyanyasaji wa kingono au unyanyasaji wa kijinsiya.

Utapewa usaidizi wa kuimarisha ustawi wako na kukusaidia kupona.

Hutabaguliwa kwa sababu ya rangi yako, kabila, utaifa, mawazo, dini, imani, jinsia, luga, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, umri, afya, ulemavu, hali ya kuishi au misingi yoyote.

***Haki zako kama mwafirika wa unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kijinsia:***





# 1. Haki kwa heshima

**A.** Utatendewa vyote kwa adabu na huruma, kupitia kiufundi halisi na haki.

**B.** Utamaduni wako, maadili na maoni yako yataheshimiwa. Mahitaji yako binafsi na chaguo lako zitazingatiwa kama ya muhimu sana.



# 2. Haki ya kupata usaidizi na musaada

a. Una haki ya kupokea usaidizi na msaada kulingana na mahitaji yako binafsi.

b. Kwa kupata usaidizi na msaada hautegemee kama, wala vipi, wewe hushirikiana na uchunguzi wowote au ushirika au mchakato wa uwajibikaji.

c. Ikiwa unahitaji na kuitaka, Umoja wa Mataifa utakusaidia kutafuta na kupata usaidizi wa haraka, kama vile huduma ya matunzo, mukiwemo huduma za afya ya ngono na uzazi; msaada wa kisaikolojia; maisha na usaidizi wa kimsingi kama vile chakula, mavazi, usafiri na mahali pa kuishi.

d. Ikiwa unahitaji na kuitaka, Umoja wa Mataifa utakusaidia kutafuta na kupata usaidizi wa muda mrefu, kama vile huduma ya afya, usaidizi wa kisaikolojia, upatikanaji wa usaidizi wa kisheria, msaada wa maisha na mafunzo ya ujuzi.

e. Kwa usaidizi wako wa kihisia, na kwa kuzingatia matakwa yako na maslahi yako bora, una haki ya kusindikizwa na mtu unayemwamini unapochagua au kupata usaidizi na msaada.

f. Ikiwa una umri wa chini ya miaka 18, usaidizi au huduma zozote utakazopewa zitazingatia umri wako na mahitaji yako binafsi, ikiwemo kwa mfano, kurudishwa shuleni.

g. Una haki ya kukataa aina yoyote ya usaidizi au musaada wakati wowote, ikiwemo wakati umeanza ku upokea huo musaada. Uamuzi kama huo hautakuzuia kuiomba na kuipokea baadaye.



# 3. Haki ya uhaki na uwajibikaji

a. Una haki ya kuwasilisha malalamiko ya unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kijinsia inalofanywa na wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa au wafanyakazi wanao husika kwa Umoja wa Mataifa, ambao una jukumu la kupeleka malalamiko yako kwa uchunguzi.

b. Una haki ya kutafuta uhaki na uwajibikaji kwa matatizo uliyopata kupitia michakato ya uhalifu na ya kiraia pamoja na taratibu za uongozi, za kinizamu na zisizo za kimahakama ambazo zinaweza kupatikana kwako.

c. Ukipenda, Umoja wa Mataifa utakusaidia kupata taarifa kuhusu jinsi ya kupata usaidizi wa kisheria na namna bora ya kutafuta haki na uwajibikaji, ikijumuisha katika kesi za kitaifa.

d. Iwapo ulikuwa na mtoto aliyezaliwa kwa unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kijinsia, Umoja wa Mataifa itakusaidia kupata taarifa na usaidizi wa kisheria ili kuthibitisha ubaba na madai yanayohusiana, ukipenda hivyo.



# 4. Haki ya kuamua jinsi ya kushirikishwa katika michakato ya Umoja wa Mataifa

a. Una haki ya kuamua kushiriki au kushirikiana katika michakato na mashauri yoyote ya Umoja wa Mataifa, ikiwa ni pamoja na ile inayotokana na ukweli kwamba wewe ni mwafirika wa unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kijinsia

b. Ukiamua kutoshiriki au kushirikiana katika hatua yoyote, chaguo hili linaweza kuathiri matokeo ya uchunguzi, ikijumuisha iwapo mkosaji atawajibishwa.



# 5. Haki ya kupata habari

a. Una haki ya kufahamishwa, mapema iwezekanavyo, kuhusu michakato na taratibu zinazohusika katika kuripoti matukio ya unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kinjinsia.

b. Una haki ya kupokea taarifa kuhusu huduma zote zinazopatikana ili kukusaidia. Ikiwa una mtoto aliyezaliwa kwa sababu ya unyanyasaji wa kingono au ukiukiwaji wa kinjinsia, hii itajumuisha maelezo kuhusu njia za kuanzisha kujuwa baba ya mtoto, kudai msaada wa mtoto na haki nyingine kwa mtoto wako.

c. Una haki ya kufahamishwa kuhusu hali ya mchakato wa uchunguzi na mwenendo mwingine wowote. Pia una haki ya kufahamishwa kuhusu jukumu lako na chaguzi ulizonazo katika kushiriki katika uchunguzi na mashauri mengine yoyote. Umoja wa Mataifa utakusaidia kupata na kuelewa habari hii kikamilifu.

d. Una haki ya kuomba kwamba taarifa itolewe kwako katika luga unayoelewa, na kwa njia ambayo iko wazi na kupatikana kwako, kwa kuzingatia hali yako ya kibinafsi, kama vile ulemavu wowote wa kusikia, kuona au kiakili. Ikiwa una umri wa chini ya miaka 18, una haki ya kupokea taarifa kwa njia inayozingatia umri wako.





# 6. Haki ya kusikilizwa

a. Una haki ya kutoa maoni yako juu ya suala lolote linalohusiana na haki hizi, na kusikilizwa na kukusikia. Pia una haki ya kutetea kwa niaba yako mwenyewe na kutambulisha mahitaji yako. Unachosema kitazingatiwa katika maamuzi au hatua zozote zinazofanywa na Umoja wa Mataifa ambazo zinaweza kuathiri usalama wako, utu au ustawi wako au wale walio karibu nawe.

b. Kwa msaada wako wa kihisia na wa vitendo na kwa kuzingatia matakwa yako na maslahi yako bora, una haki ya kusindikizwa na mtu unayemwamini, katika taratibu zozote za uchunguzi, maongezi na mikutano. Unaweza kusindikizwa na mwakilishi wa kisheria katika hali fulani.

c. Una haki ya kuwa na mahitaji yako binafsi na hali ya kibinafsi ambayo inaweza kuathiri uwezo wako wa kutekeleza ipasavyo haki yako ya kusikilizwa kuzingatiwa. Ikiwa una umri wa chini ya miaka 18, una haki ya kuwa na taratibu zozote za uchunguzi, mahojiano au mikutano inayofanywa kwa njia inayozingatia umri wako. Una haki ya kuchagua kusindikizwa na mtu unayemwamini, au la, wakati wa mojawapo ya taratibu hizi, mahojiano au mikutano.

d. Una haki ya kujumuika na kupanga na waafiriwa wengine ikiwa wewe na wao mnataka kufanya hivyo.



# 7. Haki ya faragha na usiri

a. Una haki ya kuamua, taarifa gani utatoa kuhusu hali yako kwa Umoja wa Mataifa. Huenda usingependa kutoa taarifa yoyote, au ungependa kuacha kutoa maelezo. Hii inaweza kuafiri matokeo ya uchunguzi.

b. Una haki ya siri, ingawa ukitoa taarifa yoyote ambayo inaweza kukutambulisha kwa mfanyakazi wa Umoja wa Mataifa hii inaweza kutumwa kwa wale walio ndani ya Umoja wa Mataifa ambao wanahitaji kuijua ili kuhakikisha kuwa mkosaji anawajibika. Una haki ya kuomba taarifa yoyote ambayo inaweza kukutambulisha binafsi isitolewe kwa wahusika inje ya Umoja wa Mataifa.

c. Una haki ya kuambiwa matumizi yaliyokusudiwa ya taarifa yoyote unayoamua kutoa, ikijumuisha nani taarifa hii inaweza kufichuliwa. Unapaswa kufahamishwa kwamba chaguo lolote la kuweka habari kuwa siri linaweza kupunguza ukweli wa uchunguzi, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kumwajibisha mkosaji. Uamuzi wako wa kutotoa taarifa hautaafiri haki yako ya kupokea musada na usaidizi.

d. Una haki ya kufahamishwa na Umoja wa Mataifa kuhusu uchunguzi na matokeo yoyote yanayoweza kusababishwa na malalamiko yako kwa usalama wako na wale walio karibu nawe.



# 8. Haki ya kulindwa

a. Kukuweka salama ni muhimu sana kwa Umoja wa Mataifa. Unyanyasaji wowote, vitisho, na kulipiza kisasi kwa kuripoti kile kilichotokea kwako, yanayowakabili wewe au wale walio karibu nawe, au mashahidi wowote kwa niaba yako, haukubaliki. Ukiripoti vitendo kama hivyo kwa Umoja wa Mataifa, itachukua hatua ili kulinda usalama wako wa kimwili na kulindwa shida ya kisaikolojia au kuzalauliwa, kwa mujibu wa matakwa yako, kwa kufanya kazi na mamlaka za Serikali au mashirika yasiyo ya kiserikali.

b. Umoja wa Mataifa utafanya kila linalowezekana kukulinda zidi ya mawasiliano yoyote na mtuhumiwa wakati wa kesi zinazoendeshwa na Umoja wa Mataifa.

c. Umoja wa Mataifa utashirikiana na wana inchi kutafuta kwamba hatua za ulinzi zinapatikana katika kesi zozote za kitaifa





# 9. Haki ya kukata rufaa

a. Wahalifu wanawajibika kibinafsi kwa vitendo vya unyanyasaji wa kingono na ukiukiwaji wa kijinsia . Una haki ya kutafuta masuluhisho kutoka kwao ambayo yanakiri madhara uliyoyapata na kusaidia kuyarekebisha. Masuluhisho ambayo unastahiki yatategemea sheria ya nchi ambapo kesi yako inachunguzwa au kusikilizwa na inaweza kujumuisha fidia ya kifedha; ukarabati wa kimwili na kisaikolojia na msaada wa nyenzo; kuomba msamaha; au hatua za kuhakikisha kuwa hakuna marudio ya kosa.

b. Ikiwa ubaba wa mtoto aliyezaliwa kwa sababu ya unyanyasaji wa kingono ao ukiukiwaji wa kijinsia umehakikishwa , una haki ya kuleta kesi dhidi ya baba ili kumtaka akubali jukumu lake la mzazi, ikiwa ni pamoja na kumlazimu kutoa msaada wa mtoto kulingana na taifa husika. sheria ya nchi ambapo kesi yako imeamuliwa. Mtoto wako anaweza kudai haki zaidi, kama vile utaifa au uraia wa baba. Umoja wa Mataifa utakusaidia katika michakato hii na kufanya kazi na Nchi husika ili kuwezesha utatuzi wa haki na haki wa madai haya.



# 10. Haki ya kulalamika kuhusu huduma uliyopata

a. Ikiwa unaona kuwa haki katika hati hii hazijaheshimiwa na Umoja wa Mataifa, una haki ya kulalamika kwa Ofisi ya Wakili wa Haki za Waathiriwa. Sambamba na matakwa yako, malalamiko yako yatazingatiwa na utafahamishwa hali ya hatua yoyote iliyochukuliwa kujibu.

b. Utalindwa zidi ya kisasi kutoka kwa Umoja wa Mataifa ikiwa utalalamika.



Wasiliana na Ofisi ya Wakili wa Haki za Waathiriwa kwa: ovra@un.org.